



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



## HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

*Barua zote zjandikwe na kutumwa kwa:*

Tel: +255 262 965 732 (Direct line)  
e-mail: [ded@sikongedc.go.tz](mailto:ded@sikongedc.go.tz)  
Tovuti: [www.sikongedc.go.tz](http://www.sikongedc.go.tz)

Mkurugenzi Mtendaji (W)  
S.L.P. 70,  
SIKONGE,  
TABORA.

13/07/2020

### TANGAZO LA KAZI ZA UJENZI WA KIWANDA CHA KATI CHA KUCHAKATA NA KUFUNGASHA MAZAO YA NYUKI.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikunge imepata fedha kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania kwa ajili ya Ujenzi wa Kiwanda cha Kati cha Kuchakata na kufungasha Mazao ya Nyuki.

Kwa kuwa njia ya ujenzi inayotumika ni ya kutumia wataalamu wa ndani na kununua vifaa (Force Account); Hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikunge anawatangazia Wananchi wote, (Mafundi Wenyeji); wenye uwezo na sifa zilizotajwa hapo chini watume maombi yao kwa ajili ya Ujenzi huo:-

- i. **Awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka kumi na nane (18) Mwenye Ujuzi na Uzoefu wa kazi za Ufundu Ujenzi anayeishi Mkoa wa Tabora; (Mafundi wenye sifa wanaoishi Wilaya ya Sikunge watapewa kipaumbele).**
- ii. **Awe na uwezo wa kusoma na kutafasiri michoro, vipimo na uwiano wa vifaa vyta ujenzi.**
- iii. **Aoneshe majengo yasiyopungua mawili (2) ya serikali, aliyojenga ndani ya Mkoa wa Tabora.**
- iv. **Asiwe na historia ya kudhulumu, kutapeli au kutowalipa mafundi anaoshirikiana nao au kushindwa kukamilisha kazi alizowahi kupewa.**
- v. **Aoneshe ni kwa muda gani atamaliza ujenzi wa jengo analoomba kulijenga.**

Aina ya kazi zitakazo fanyika Katika Ujenzi wa Kiwanda cha Mazao ya Nyuki ni pamoja na:

- A. Kujenga Msingi wa jengo (Sub-structure)
- B. Kunyanya jengo (Super-structure)
- C. Kuezeka (Roof structure and covering)
- D. Kusimika fremu na kufunga Milango
- E. Umaliziaji(finishing)
- F. Rangi na Mapambo (Painting & Decoration)
- G. Umeme (Electrical installation)
- H. Mifumo ya maji safi na taka (water supply and sewage system)

## 1. MENGINEYO

- i. Waombaji wanatakiwa kuja kuchukua BOQ na michoro ya jengo linaloombwa kujengwa katika Ofisi ya Ugavi na Manunuzi mara baada ya kulipia kiasi cha T.Sh 15,000.00 katika benki; (Mwombaji afike ofisi ya Mweka hazina wa Wilaya ili apewe bill na akaunti ya kulipia.
  - ii. Maombi yote yawekwe kwenye bahasha na kufungwa na juu ya bahasha iandikwe kazi iliyoombwa kama ilivyofafanuliwa hapo juu
  - iii. Maombi yote yaandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge na kuwasilishwa katika Ofisi ya Ugavi na Ununuzi, Halmashauri ya Wilaya Sikonge
  - iv. Vifaa vyote vitakavyotumika katika ujenzi husika vitanunuliwa na Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Sikonge
2. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Maombi ni tarehe 20/07/2020, Jumatatu saa 4.30 Asubuhi. Usahili utafanyika kwa kila mwombaji siku hiyo ilikupata mafundi wenye sifa stahiki.

Imetolewa na;

Tito E. Luchagula

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**SIKONGE**

MKURUGENZI MTENDAJI  
WILAYA - SIKONGE